

SHIRIKA LA RELI TANZANIA

Simu: 2133990
Telegramu: Railways
Nukushi: 2133428



Ofisi ya Uhusiano
S.L.P 70364
Dar es Salaam

TAARIFA KWA UMMA TRC INAKEMEA UNYANYASAJI WA WAFANYAKAZI KATIKA KAMBI ZA SGR

Dar es Salaam, Tarehe 25 Machi 2023.

Shirika la Reli Tanzania – TRC linautaarifu umma kuwa mnamo tarehe 18 Machi 2023 lilitokea tukio la kushambuliwa kwa mfanyakazi wa mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa – SGR aitwaye Lucy Paulo mwenye fani ya upishi katika kambi ya mradi wa SGR Fela mkoani Mwanza.

Lucy alishambuliwa na raia wa taifa la China aitwaye Bwana Zheng Yuan Feng majira ya saa tatu kasoro asubuhi eneo la jikoni kwa kumtolea lugha chafu na kumpiga kitendo hiki kilipelekea Lucy kupata majeraha na kupelekwa hospitali ya Bugando na Siku ya Jumatatu tarehe 20 Machi 2023 alipatiwa matibabu na kuruhusiwa siku ya Jumanne ya tarehe 21 Machi 2023 majira ya asubuhi na kwasasa yupo kambini ya Fela chini ya uangalizi wa Daktari wa mradi.

Kufuatia tukio hilo Bwana Zheng alikamatwa na kuzuiliwa kwenye kituo cha Polisi Reli na baadaye kuhamishiwa kituo cha Polisi wilaya ya Misungwi, Mnamo tarehe 24 Machi 2023 alipandishwa katika mahakama ya Wilayani Misungwi na Kusomea Mashtaka yake kwa kosa la kujueruhi kesi Na 44 ya mwaka 2023. Kwasasa yupo rumande katika kituo cha Polisi Misungwi baada ya kushindwa masharti ya dhamana.

TRC imemtaka Mkandarasi kampuni ya CCECC-CRCC kuhakikisha Lucy Paulo anapatiwa stahiki kwa kufuata sheria, taratibu na kuhakikisha anafanya kazi kwa uhuru wakati wote wa mradi, mkandarasi ameridhia kutekeleza matakwa hayo na TRC itaendelea kufatilia.

Shirika linakemea kitendo hicho na vitendo vya aina yoyote vyenye lengo la kuleta uonevu na unyanayasaji kwa wafanyakazi na kuwataka wakandarasi kufatilia nyendo zote za wafanyakazi na kuchukua hatua kwa mujibu wa Sheria za nchi na matakwa ya kimkataba.

A handwritten signature in black ink.

Jamila Mbarouk
Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano